OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

HOTUBA YA MGENI RASMI MH. DKT. JUMA ZUBERI HOMERA (MB) WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA, KATIKA KIKAO CHA WATUMISHI WOTE WA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI KILICHOFANYIKA JIJINI ARUSHA KATIKA HOTELI YA LUSH GARDEN TAREHE 28 APRILI, 2026

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Johari,
Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Bw. Samweli Maneno,
Wakurugenzi wa Divisheni,
Wakuu wa Vitengo
Wakurugenzi Wasaidizi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,
Watumishi Wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
Wageni waalikwa,
Mabibi na Mabwana,

Nawasalimu wote kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Ikiwa ni mara yangu ya kwanza kukutana nanyi Watumishi wa Ofisi hii nyeti ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha wote kuamka salama na kukutana leo hii katika kikao hiki cha Watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Sifa na Utukufu vimrudie yeye.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni moja ya Ofisi nyeti sana katika Taifa letu. Ni moja ya Ofisi chache zilizoanzishwa na Katiba ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kukasimiwa jukumu zito la kuwa mshauri wa mwisho wa Serikali katika masuala ya kisheria.
Napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwenu kwa namna mmekuwa mkitekeleza jukumu hili zito la kikatiba. Maendeleo ambayo Taifa letu imeyapata hadi leo hii hayawezi kuzungumziwa bila kutaja mchango wenu nyie Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hongereni sana kwa mchango mkubwa mnaoutoa katika maendeleo ya Taifa letu.

Ndugu Watumishi

Napenda pia kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ndug. Hamza Johari, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Ndug. Samweli Maneno na Menejimenti yote ya Ofisi hii kwa namna ambavyo mnatekeleza majukumu yenu kwa Ufasaha na kuifanya Ofisi yenu kuendelea kuwa nguzo imara ya maendeleo ya Taifa letu. Bila Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imara hapawezi kuwa na Taifa au Nchi Imara. Hongereni sana kwa kweli.

Nimetaarifiwa kuwa mmefanikisha mkutano wenu wa Baraza la Wafanyakazi vizuri. Napenda kuwapongeza kwa jambo hili, ni matarajio yangu kuwa mmezungumza kwa uwazi namna mnavyopaswa kuboresha mambo yanayowahusu ikiwemo maslahi yenu, utendaji kazi wenu pamoja na masuala mengine yote yanayowahusu. Ni matumaini yangu pia kuwa mmejipanga vizuri juu ya namna ya kuzikabili vizuri changamoto zote zinazowakabili.

Ndugu Watumishi

Nafahamu kuhusu changamoto za maslahi zinazowakabili. Sisi kama Wizara kwa kushirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali tutaendelea kujitahidi kuboresha maslahi yenu ili sio tu muwe na maisha mazuri bali

muwe na furaha katika kutekeleza majukumu yenu jambo litakalochochea ufasaha wa kazi zenu. Tarehe 30 Juni 2000 aliyekuwa Waziri Mkuu wa Singapore **Lee Kuan Yu** alisema haya (**ninanukuu);**

"..... As we raced ahead and become part of the global economy, salaries of our top people were pulled up by those of their counterparts in the advanced countries. This trend is not likely to be reversed, unless we go into decline, in which case, the well trained and highly skilled will leave, accelerating our fall, So I advised and persuaded the Prime Minister to take this Formula of automatic adjustment to the Parliament"

Ni ukweli usiopingika kuwa, usipozingatia vizuri maslahi ya mtumishi anayewajibika vizuri katika masuala nyeti ya Taifa na Nchi, unaweza kuanguka kama Taasisi au Nchi maana mtumishi huyo anaweza kushawishiwa kuondoka na Kwenda sehemu nyingine ambayo atalipwa vizuri na kuhamishia utaalamu wake sehemu nyingine. Kama Wizara tutazidi kulizingatia suala la maslahi yenu ili Nchi yetu na Taifa kwa ujumla tuzidi kunufaika na utaalamu wenu.

Ndugu Watumishi

Najua wote mnafahamu kuwa katika maisha yenu hapa duniani, mnatumia muda mwingi mkiwa makazini kuliko mnavyokuwa majumbani kwenu na familia zenu. Hivyo sitakosea nikisema katika utumishi wenu, familia yenu ya kwanza ni nyie watumishi mnaofanya kazi pamoja.

Kwa sababu hiyo, napenda kuwahusia masuala yafuatayo katika kuishi kwenu pamoja na kufanya kazi kwa moja;

Kwanza ni Kupendana

Katika dunia hii ya leo, ukitaka kuishi kwa amani na furaha ni vizuri wote mkaishi kwa kupendana. Panapokuwa na upendo kuna amani, na pale kwenye amani kuna furaha. Maisha ya utumishi yana changamoto nyingi. Bila kupendana hamtaweza kufanya kazi kwa furaha na amani. Epukeni kutengenezeana ajali, epukani kufanyiana mabaya. Duniani tuna muda mchache sana wa kuishi, hivvyo ni vizuri tukaishi kwa kupendana na kujaliana.

Pili kufanya kazi kama Team,

Katika maisha siku zote wekeni kipaumbele kufanya kazi kama Team moja. Kuanguka kwa mmoja wenu kuchukuliwe kama kuanguka kwenu wote. Mafanikio ya kila mmoja wenu ndiyo mafanikio ya Ofisi. Na Ofisi ikifanikiwa, Taifa limefanikiwa. Kamwe msione sawa mmoja wenu anapoanguka au kushindwa kutekeleza majukumu yake.

Tatu kila mtu awe kiongozi wa mwenzake.

Aliye mdogo kuliko wote amuheshimu mkubwa wake, vivyo hivyo yule mkubwa awaheshimu wadogo. Msiogope kukosoana na kufundishana maana kupitia hayo ndivyo mtaweza kuboresha utendaji kazi wenu. Mmoja wa waasisi wa Taifa la Marekani na Mwanasayansi maarufu **Benjamin Flanklin** aliwahi kusema; **ninanukuu**

“..... critics are our best friends because they tell us our faults”

Kwa tafsiri ya kiswahili cha kawaida kabisa maneno haya yanamaanisha **ukosoaji ni rafiki yetu mkubwa maana unatueleza mapungufu yetu.**

Rai yangu kwenu ni kwamba katika kufanya kwenu kazi, chukulieni kukosoana kama sehemu ya kufundishana. Kikubwa mkosoane kwa staha na heshima mkiwa na nia njema ya kufundishana na kujengana vizuri.

Nne Uadilifu.

Naelewa uadilifu ni somo linalofundishwa sana katika utumishi wa umma. Hata mimi leo napenda kuwahusia katika hili. Mmesikia kilichosemwa na ripoti ya Jaji Chache kuwa moja ya mambo yaliyosababisha vurugu za uchaguzi mkuu uliopita ni malalamiko ya wananchi kuhusu uadilifu wa viongozi wa umma na watumishi wa Serikali. Ni vizuri kuzidi kujitathmini kuwa tunapaswa kuwa waadilifu ili tusisababishe manung'uniko kwa wananchi na kuhatarisha amani na usalama wa Taifa letu.

Tano msiache kuwekeza.

Katika kufanya kwenu kazi, ni vizuri mkakumbuka kuwa utumishi wa umma una mwisho na maisha lazima yaendelee baada ya kumalizika kwa utumishi wa umma. Ni vizuri mkiwa kazini mkaangalia fursa mbalimbali za uwekezaji zinazopatikana. Wekezeni kwenye biashara, bonds na maeneo mengine ili kujihakikishia mnaishi maisha mazuri hata baada ya kumalizika kwa utumishi wenu wa umma.

Mwisho ni Kujiendeleza Kitaaluma na Kimaarifa

Nafahamu kuwa wote hapa mnafahamu kuwa, msingi mkuu wa maendeleo ya Taifa lolote lile duniani ni mifumo imara na wezeshi ya kisheria inayochochea ukuaji mkubwa wa Uchumi.

Taifa letu limezindua rasmi Dira Mpya ya Maendeleo ya Miaka 25 ambayo tunaanza kuitekeleza rasmi kuanzia mwaka huu mpya wa fedha. Napenda kutoa rai kwenu mzidi kujiendeleza kitaaluma na kimaarifa ili muweze kulishauri vizuri Taifa letu hasa juu ya Sheria zipi zinapaswa kutungwa na kurekebisha kwa ajili ya kuchochea vizuri ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kweli kwa Wananchi wote.

Kuna nchi duniani hazina bahari, hazina mbuga za wanyama, hazina madini wala gesi ila zina maendeleo makubwa sana kutokana na mifumo tu ya kisheria inayochochea uwekezaji na biashara. Ni maombi yangu kwenu kuwa ni vizuri sasa mkajikita katika kujipa maarifa mapya ili nchi yetu iingie kwenye ramani ya moja ya Nchi zenye maendeleo makubwa zaidi duniani kupitia mifumo mizuri na imara ya kisheria itakayotokana na ushauri wenu mzuri.

Hitimisho

Ndugu Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nipende kuwashukuru tena kwa kuona umuhimu kwa mimi kuja kushiriki tukio hili lenu muhimu la mkutano wenu. Kama Wizara hatutaacha kupigania maslahi yenu kama sehemu ya Watumishi wa Taasisi zilizo chini yetu. Nipende kusisitiza mzidi kuwa wazalendo kwa kulipenda kweli Taifa lenu la kulishauri vizuri katika ukweli na weredi ili lizidi kustawi na kuwa na amani na utulivu maana bila amani na utulivu hapawezi kuwa na maendeleo ya kweli.

Asanteni kwa kunisikiliza

Mungu awabariki sana

Mungu ibariki Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali